(03)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

**MKOA WA KATAVI**
Anwani ya Simu: "AFYA", KATAVI
Simu ya Mdomo: 025–252957128
Fax No. 025- 252957129

Hospitali ya Rufaa Mkoa,
S. L. P. 449,
**KATAVI**

## MKATABA WA UJENZI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA KATAVI

### Mkataba na ME.007/KTVRRH/2021/2022/G/3

Mkataba huu umefikiwa leo hii tarehe 05.. mwezi 01.. Mwaka 2022 hapa Mpanda, **KATI YA MKURUGENZI WA HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA KATAVI** (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MWAJIRI**) kwa upande mmoja na **ELDARD BASHASHA KAPOCHO S.L.P 94 MPANDA** (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **Fundi Mchundo** Mwajiriwa kwa upande mwingine).

**NA**

**Kwakuwa, Mwajiri anahitaji mtoa huduma ya Ufundi na vifaa vya Chumba cha Telemedicene kwa shilingi Tsh milioni kumi (10,000,000)** bila **VAT**

Na kwakuwa, mtoa huduma ya ukarabati anao ujuzi, uwezo na uzoefu wa kutoa huduma kwa taasisi za serikali na ana nia ya kutekeleza kazi tajwa.

**Hivyo basi,** Mwajiri na Mwajiriwa wanakubaliana yafuatayo;

1. Kwamba, m**alipo kwa mwajiriwa yatafanywa na mwajiri mara baada ya mtoa huduma ya ukarabati wa chumba cha telemedicine kutoa huduma hiyo kwa ukamilifu na baada ya kukaguliwa na kukubaliwa na mwajiri.**
2. Kwamba, hakutakuwa na malipo ya awali katika mkataba huu.
3. Kwamba,upande wowote unaweza kuvunja mkataba huu kwa notisi ya maandishi ya siku 7 ya kusudio la kuvunja mkataba kwa upande mwingine ikiwa upande mwingine utashindwa kutekeleza masharti ya mkataba huu
4. Kwamba,ikitokea upande wowote haujatekeleza wajibu wake ipasavyo,pande zote mbili zitakutana ndani ya siku (2) ili kuona namna bora ya upande ambao haujatekeleza wajibu wake na kutekeleza wajibu huo ipasavyo.
5. Kwamba,jukumu la usalama na wa eneo la kazi litakuwa ni la mwajiriwa mpaka pale atakapokabizi kazi hiyo kwa mwajiri.
6. Kwa kuwa mkataba huu umeingiawa kwa nia njema na kwa manufaa ya pande mbili,iwapo kutatokea mgogoro au kutokuelewana kokote katika utekelezaji wa mkataba huu basi MSULUHISHI anayekubalika na upande zote atatafutwa ili kusuluhisha mgogoro huo.iwapo muafaka hautapatikana basi suala hilo litapelekwa mahakamani.

7. Kwamba mkataba huu unatawaliwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MKATABA huu umetiwa saini leo na hawa wafuatao;

**MWAJIRI**

JINA: GEORGE MWAMBENE

CHEO: KAIMU MGANGA MFAWIDHI

ANWANI: 449,

SAHIHI: [signature] TAREHE: 05-01-2022

Kny: MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA
S.L.P. 216
KATAVI

**MBELE YA**

JINA: EMMANUEL TINAA

CHEO: AG HS

ANWANI: 449 MPANDA

SAHIHI: [signature] TAREHE: 05/01/2022

**MTOA HUDUMA**

JINA: ELDARD B KAPOCHO

CHEO: MD

ANWANI: BOX 94,

SAHIHI: [signature] TAREHE: 05.01.2022

ELDARD BASHASHA KAPOCHO
P.O.Box 94
TIN : 103-962-153
MPANDA KATAVI

**MBELE YA**

JINA: JULIAS MAICAL

CHEO: FUNDI

ANWANI: 94,

SAHIHI: [signature] TAREHE: 05/01/2022